# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**MEI, 2026**

**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**


70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz


# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo ili kutekeleza majukumu na wajibu wetu wa kikatiba kwa manufaa ya wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, ninatoa shukrani za dhati kwako binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama Kanuni ya 103 (6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2024 kuhusu **Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake thabiti na juhudi anazoendelea kuzifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Sisi sote ni mashahidi kuwa chini ya uongozi huu kumekuwa na mageuzi mbali mbali katika miradi ya maendeleo ya kisekta ikiwemo uchumi, miundombinu, afya, elimu jambo ambalo linaonesha dhamira ya kweli ya kujenga Zanzibar yenye ustawi na mafanikio makubwa zaidi. Ni matumaini ya kamati kuwa juhudi hizi zitaendelea kuimarika zaidi

na kuleta matokeo chanya kwa wananchi wote kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu inatambua na kuthamini mchango aliutoa Mheshimiwa Othman Masoud Othman katika kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kipindi chote alichotumikia katika nafasi yake ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa hakika msaada wake ulikuwa wenye kujenga na kuimarisha nchi kwa maslahi ya Taifa hili.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kupongeza juhudi za Mheshimiwa Kaimu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Hamza Hassan Juma na wizara nzima kwa juhudi zao kubwa wanazoendelea kuzifanya katika kutekeleza majukumu yao. Ushirikiano huo ulihusisha utoaji wa taarifa muhimu, ziara za uchunguzi, pamoja na kupata ufafanuzi juu ya masuala mbali mbali yaliyoibuliwa na kamati. Aidha, kamati inatoa shukrani kwa wadau wote wa taasisi za Serikali na zisizo za Serikali kwa mchango wao endelevu kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Sambamba na hilo, kamati imetambua mchango kutoka kwa watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na ni matumaini ya kamati kuwa wizara itahakikisha inaboresha changamoto zilizopo ikiwemo ya mfumo ili kuhakikisha shughuli za kiutendaji zinaendelea bila ya vikwazo. Kwa muktadha huo, kamati inaamini utatuzi wa changamoto hizo utasaidia kuongeza uwazi, uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutambua na kuthamini mchango uliotolewa na wajumbe katika kipindi chote cha utekelezaji wa kazi za kamati, kila mjumbe alionesha ushirikiano uliowezesha kamati kukamilisha kazi zake. Kamati inawashukuru wajumbe wote kwa ushiriki wao kikamilifu katika vikao, kutoa maoni yenye kujenga, kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa mbali mbali pamoja na kushiriki katika ziara za ukaguzi zilizofanyika katika maeneo

tofauti ya utekelezaji wa shughuli husika. Hakika, ushiriki wao uliimarisha ubora wa ripoti hii na kuipa mwelekeo sahihi. Kwa mantiki hiyo naomba kuwataja kwa majina ya Waheshimiwa Wajumbe waliounda kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Aza Januar Joseph | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mahfoudh Abdalla Mohamed | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Masoud Amour Masoud | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mahmoud Shineni Ali | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mmanga Mohammed Hamed | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kamati pia, inathamini msaada kutoka kwa makatibu kamati katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi, kufanya mawasiliano na wadau mbali mbali na kuhakikisha taarifa zote zinapatikana kwa wakati. Hii ni wazi kwamba ubora wa ripoti hii kwa kiasi kikubwa umetokana na juhudi zao katika kuhakikisha shughuli zote za kamati zinaendeshwa kwa mpangilio na kwa kuzingatia kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi za Mwaka 2024. Kwa ruhusa yako naomba kuwataja makatibu hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 2. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 3. | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| 4. | Ndg. Hassan Lila Mrisho | Afisa bajet |
| 5. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ni moja ya kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu 119(1) katika jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya Mwaka 2024 kwa lengo la kusaidia Baraza lako Tukufu

kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kushauri na kuikagua Serikali. Kwa mazingatio hayo, kamati ilipitia, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027, tarehe 22 Aprili 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kusimamia maeneo makuu manne ya kiutekelezaji kupitia mafungu matano ya bajeti ambayo ni **Fungu 002 (Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais), Fungu 032 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya), Fungu 033 (Tume ya UKIMWI) na Fungu 034 (Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira).**

**Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, kwa mujibu ya Kanuni ya 103(6) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024 na kwa niaba ya kamati naomba niwasilishe mbele ya Baraza lako Tukufu maoni kuhusiana na mafungu ya bajeti ya wizara hii kupitia Programu Kuu na Programu ndogo zilizomo kama ifuatavyo:

**PROGRAMU KUU YA URATIBU WA MABADILIKO YA TABIANCHI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kifungu cha 22 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar Nam. 2015, moja ya athari zinazoikumba nchi zinazoendelea ni athari za mabadiliko ya tabianchi, ambazo huathiri moja kwa moja sekta mbali mbali ikiwemo Sekta ya Miundombinu, Sekta ya Afya, Sekta ya Kilimo, Sekta ya Mifugo nakadhalika. Kamati kupitia Baraza hili, inaiomba Serikali kuweka sera maalumu za kukabiliana na changamoto, kufanya juhudi za utoaji elimu kwa umma ikiwa ni pamoja na kufanya kampeni endelevu juu ya uelewa wa athari za tabianchi, kuingiza elimu ya mazingira katika mitaala ya skuli, kutoa motisha kwa wawekezaji wa nishati safi pamoja na kuimarisha sheria kali dhidi ya uchafuzi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** fungu 002 – Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuthamini umuhimu wa kifungu kidogo cha **S0101 cha Uratibu na Mabadiliko ya Tabianchi** kamati inatambua kuwa mabadiliko hayo ni tishio kubwa kwa maendeleo endelevu. Kupitia ripoti hii, kamati inaiomba Serikali kuweka mpango madhubuti, usimamizi bora na kutoa ushirikiano kwa wadau wote. Kwa kufanya hivyo, Taifa linaweza kupunguza athari na kujenga taswira bora kwa vizazi vya sasa na vijavyo, kwani suala la mazingira sio la Serikali peke yake bali ni jukumu la kila mwananchi, sekta binafsi na jamii kwa ujumla.

**PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA WATU WENYE ULEMAVU**

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu, ni sehemu muhimu ya jamii yetu na inapaswa kupewa kipaumbele. Kwa kuliona hili, kamati inatoa wito kwa Serikali na wadau wote wa maendeleo kuendelea kuimarisha sera na mipango inayolenga kuwawezesha kupatia elimu, ajira, huduma za afya na fursa za kiuchumi katika hali ya usawa. Vile vile kamati inaendelea kusimamia na kutetea haki za watu wenye ulemavu kwa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu na kuhakikisha mazingira ya taasisi za umma na binafsi yanafanywa rafiki kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na miundombinu bora na huduma jumuishi zinazozingatia mahitaji maalum.

**PROGRAMU KUU YA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA**

**Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa **fungu la 032** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka 2026/2027, limeainisha kuwa licha ya Serikali kupiga hatua juu ya udhibiti wa dawa za kulevya, lakini bado tatizo la usambazaji na uuzwaji wa dawa za kulevya limeendelea kuwa changamoto kubwa inayogusa afya ya jamii, usalama wa taifa na mkwamo katika maendeleo ya kiuchumi. Kamati imebaini ongezekezo la uingizwaji wa mirungi kwa bandari bubu katika Mkoa wa Kaskazini Pemba

ikizingatia kuwa vitendo hivyo ni kinyume na sheria na pia vinahatarisha usalama, afya na ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika,** ingawa juhudi za Serikali katika kulinda fukwe dhidi ya uingizwaji wa dawa za kulevya zimeendelea kupiga hatua siku hadi siku, lakini bado zinahitaji kuimarishwa zaidi kupitia teknolojia pamoja na ushiriki wa wana jamii kwani kupambana na janga hili ni jukumu la pamoja kati ya Serikali na wananchi. Aidha, kamati inapendekeza mamlaka hii kuongeza doria, kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kuweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji ili kukomesha vitendo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kifungu cha P02 cha Udhibiti wa Dawa za Kulevya, kamati inaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha **TZS Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Mbili na Sabiini na Nne, laki Nne na Sitini Elfu. 13,274,460,000/=** kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar ili ziweze kuimarisha operesheni za upelelezi, doria za udhibiti, pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya Dawa za Kulevya. Sambamba na hilo, kamati inapendekeza kuwepo kwa uwekezaji zaidi katika mafunzo ya wataalamu, ununuzi wa vifaa vya kisasa, pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya vyombo vya ulinzi na usalama ili kuongeza ufanisi katika mapambani dhidi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia suala zima la udhibiti wa dawa za kulevya, kamati imebaini ongezeko kubwa la dawa za kulevya linatokana na njia mpya ya uingizwaji wa dawa hizi kwa mfumo wa vidonge vya dawa tiba. Kamati inatoa ushauri kwa mamlaka husika kuendelea kufanya operesheni za mara kwa mara kwa taasisi zote zinazohusiana na uingizwaji wa dawa tiba ikiwemo Bohari Kuu, ZFDA na Ofisi ya Mkemia Mkuu. Pamoja na hayo, kamati imeitaka mamlaka kuongeza nguvu ya utoaji elimu kwa wafamasia juu ya namna bora na sahihi ya utoaji dawa tiba na athari zinazoweza kutokezea pindipo dawa hizo zitatumika kinyume cha sheria.

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla kamati inatambua, kusifu na kuthamini juhudi za mamlaka hii, kwa kuonesha ithibati ya kazi nzuri inayofanywa ikiwa ni pamoja na kufanya operesheni 28 kwa dawa za kulevya, lakini bado inaendelea kutoa msisitizo juu ya suala la ushirikiano mzuri baina ya taasisi za ndani na za kimataifa na kuwataka jamii kutokua na muhali wa kutoa taarifa za uhalifu na badala yake ishirikiane kikamilifu na vyombo vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha taifa letu linaendelea kuwa salama na lenye nguvu kazi yenye afya.

**PROGRAMU KUU YA URATIBU MUITIKO WA TAIFA WA UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika,** ni wazi kuwa dhamira ya kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora ya afya bila ya ubaguzi ni ishara tosha kuwa Serikali imejipanga kutokomeza maambukizi mapya ya VVU ifikapo 2030. Kamati imedhibitisha hili, kupitia **kifungu P02 cha Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI** ambapo inaiomba Serikali kuhakikisha sera, mipango na mikakati yote iliyowekwa inatekelezwa kwa ufanisi katika ngazi zote za mikoa na wilaya. Hata hivyo, kamati inaendelea kusisitiza Serikali juu ya umuhimu wa elimu ya kinga, uboreshwaji wa huduma bora za afya pamoja na kuondoa kabisa unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na VVU ili kuhakikisha haki na utu wa kila mwananchi unalindwa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia **kifungu kidogo cha S0202 Mawasiliano na Utetezi Juu ya Masuala ya UKIMWI**, kamati inapendekeza Tume kuimarisha na kupanua ushirikiano kwa taasisi za elimu na vyombo vya habari katika kueneza ujumbe sahihi kuhusu UKIMWI. Kwa kufanya hivyo, kamati inaamini kuwa juhudi za kitaifa katika mapambano dhidi ya UKIMWI zitazidi kuimarika na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa msingi huo, kamati ina imani kuwa uidhinishwaji wa fedha kwa **fungu 033** utawezesha Tume kuimarisha shughuli na harakati za kuelimisha jamii, ikiwa ni pamoja na

uboreshwaji wa huduma katika ngazi zote za wilaya, hatua ambayo ni muhimu katika kuhakikisha malengo ya kitaifa yanafikiwa.

**PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

**Mheshimiwa Spika,** kwenye **fungu 034 la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar,** kamati inaiomba Serikali kutafuta ufadhili wa miradi ya kimazingira pamoja na kupanua dhana na ushirikiano na mashirika ya kimataifa ili kuongeza ufanisi katika uhifadhi wa mazingira. Kimsingi, kamati imeona ipo haja ya wazanzibari kushiriki katika mikutano ya kimazingira kama nyenzo muhimu kwa maendeleo endelevu. Jambo hili litaiwezesha Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kukabiliana vyema na changamoto za kimazingira.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ufinyu wa jengo la ofisi kwa mamlaka hii na Idara ya Mazingira kwa upande wa Pemba, kamati inaomba Serikali kulitafutia suluhisho suala la upatikanaji wa eneo ili kuiwezesha mamlaka hii kutekeleza majukumu yake kwa tija zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuhamasisha matumizi mbadala ya mifuko ya plastiki, kudhibiti uingizwaji wake na kuweka mazingira katika hali ya usalama. Katika kufanikisha azma hii, wizara kupitia **kifungu kidogo cha S0201 Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria,** kamati imeona ipo haja kwa Serikali kuweka sheria mpya ya kuwabana wafanyabiashara wanaoendelea na matumizi ya mifuko ya plastiki pamoja na kuongeza faini kwa watu wote watakaotumia mifuko hiyo ili kulinda mazingira dhidi ya uchafuzi. Hatua hii itapelekea kujenga jamii yenye uwajibikaji wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuhitimisha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa makini wakati wa uwasilishaji

wa ripoti ya kamati na naomba wachangie mawazo yao ili kuboresha zaidi mjadala huu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taratibu nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka mpya wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

***Ahsante;***

.................................

***(Aza Januar Joseph)***

M/Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**